BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Kumi na Tisa – Tarehe 05 Juni, 2023

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa mwaka 2023/2024.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa Mwaka 2023/2024.

## III. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

189. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Kuna miradi mingi inayofadhiliwa na TASAF kupitia mpango wa Kaya Maskini, ambapo kwa sasa kumekuwa na mtindo wa kutumikisha jamii ya wazee wasiojiweza na wasio na utaalamu wowote katika kujenga barabara.

(a) Je, Serikali haioni kuwa sio jambo jema wala sio busara kwa wazee kama hao kuwatumikisha kazi kama hizo za ujenzi wa barabara kwa kisingizio cha kuwaondolea umasikini.

(b) Je, Serikali haioni kuwa ujenzi ule wa barabara usiozingatia viwango ni sehemu ya ufujaji wa bure wa pesa za Serikali na hauonyeshi umakini wa Serikali.

<u>Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:</u>

240. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:

Kwa kuwa eneo la Mkunguasi lililopo Makaani ambalo lipo karibu na mwambao wa mashariki ya kisiwa cha Pemba, katika kijiji cha Vitongoji kumekuwa na upasuaji mkubwa wa miamba kwa ajili ya kupata mawe ya kukata kokoto, jambo ambalo limesababisha uwepo wa mashimo makubwa yanayotoa maji ya chumvi na kugeuka kuwa hatari na uharibifu wa mazingira.

(a) Je, Serikali kwa kiwango gani inalitambua jambo hilo.

(b) Ni lini Wizara yako itafanya ziara ya kutembelea eneo hilo ambalo kwa kiasi kikubwa limeshageuzwa kuwa jangwa.

<u>Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:</u>

234. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Mchango wa sekta binafsi ni muhimu sana katika kukuza elimu na kuleta ushindani unaohitajika wa kuinua vipaji vya wanafunzi nchini. Hata hivyo, kuna haja kubwa kwa Serikali kuichukulia sekta hii kwa umuhimu wake.

(a) Je, kwa kiasi gani na kwa vipi Serikali inaishirikisha sekta binafsi katika masuala ya elimu.

(b) Je, kwa kiasi gani na kwa vipi Serikali inawashajiisha wawekezaji binafsi kama wadau muhimu kwenye elimu.

(c) Je, ni vivutio gani, vikiwemo vya kodi rafiki, Serikali inavitoa kwa wawekezaji bora wa elimu.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

221. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Katika mzunguko wa barabara ya Kariakoo ambayo inaunganisha barabara nne za kwa Biziredi, barabara ya kwendea chuo cha mafunzo, Kijangwani na Michenzani zimekuwa na matumizi makubwa ya vyombo vya moto. Lakini pia ni eneo ambalo limezungukwa na skuli zenye idadi kubwa ya wanafunzi pamoja na kiwanja cha kufurahishia watoto. Hata hivyo, eneo hilo halina taa za kuongozea gari na vyombo vya moto hali inayosababisha msongamano mkubwa hasa wakati wanafunzi wanapotoka skuli.

(a) Je, Serikali ina mpango wowote wa kuweka taa za kuongozea gari na vyombo vya moto ili kupunguza msongamano wa gari wakati wanafunzi wanapotoka skuli.

(b) Kwa kuwa katika eneo hilo vipo viwanja vya kufurahishia watoto, je, Serikali haioni ulazima wa kuweka taa maalumu zenye kuonesha muda wa kuvuka vyombo vya moto na watumiaji wengine wa barabara hasa watoto na watu wenye mahitaji maalumu.

(c) Katika kuepusha ajali kwa watoto wanaotoka skuli na msongamano wa gari, Je, Serikali inaweza kufanya njia mbadala wa kujenga njia maalumu za kuvukia watoto bila ya kuleta usumbufu kwa wenye vyombo vya moto.

Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

166. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Hivi karibuni nchi ya Afrika ya Kusini imetoa tamko la uhitaji wa walimu wa kufundisha lugha ya Kiswahili.

Je, ni kwa kiasi gani Serikali inazifuatilia fursa kama hizi ili wataalamu wetu wa Kiswahili waweze kunufaika nazo.

**Wizara ya Afya:**

181. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa kuwa kumekuwa na matumizi holela ya dawa za binadamu. Je, ni mkakati gani uliopo wa kudhibiti jambo hili.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

197. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Ili sekta ya mafuta na gesi asilia iweze kuleta faida kwa Serikali na wananchi, uwazi, uwajibikaji na ufanisi ni mambo ya msingi, sambamba na kuzijengea uwezo taasisi husika. Hata hivyo, bado Serikali haijayatekeleza mambo hayo kwa vitendo.

(a) Je, kwa nini hadi sasa Serikali haijazijengea uwezo wa kutosha na uhuru wa uendeshaji taasisi za mafuta na gesi asilia.

(b) Je, Serikali ina mashirikiano yepi ya karibu na taasisi za Tanzania Bara na za kikanda katika kubadilishana uzoefu wa sekta ya mafuta na gesi asilia.

(c) Je, kwa nini Serikali haijaweka wazi hatua zote zinazohusiana na masuala ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia kwa wananchi.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

20. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Serikali ya Zanzibar inatumia gharama kubwa sana ya kuwapatia wananchi wake huduma ya nishati ya umeme kutoka Tanzania Bara.

Je, ni upi mkakati wa Serikali wa kuhakikisha Zanzibar inajitegemea kupata nishati hii muhimu kwa maendeleo ya taifa kwa ujumla.

IV. **HOJA ZA SERIKALI:**

**Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa mwaka 2023/2024.

Zanzibar,
05 Juni, 2023.

(Raya Issa Msellem)
**KATIBU WA BARAZA**